JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

Dar es Salaam,

22 Novemba, 2026.

TAARIFA KWA UMMA

TUKIO LA MOTO NUNGWI, ZANZIBAR.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), inatoa pole kwa wamiliki wa biashara, wafanyakazi, wageni na wote walioathirika na tukio la moto lililotokea tarehe 21 Novemba 2026 katika eneo la Nungwi, Kaskazini Unguja. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, moto huo uliathiri hoteli sita, migahawa minne na takribani maduka 40. Wageni 183 waliondolewa salama na kuhamishiwa katika hoteli nyingine. Hakuna vifo wala majeruhi walioripotiwa.

Tukio hili linatukumbusha umuhimu wa kuchukua hatua za kuzuia majanga na kujiandaa kukabiliana na athari zake. Kuwa na kinga ya bima inayolingana na hatari zinazokabili mali au shughuli za mtu kabla ya janga kutokea husaidia kupunguza athari za kifedha na kurahisisha kurejea katika shughuli za kawaida. Haki ya kupata fidia hutegemea aina ya kinga iliyochukuliwa na masharti ya mkataba wa bima husika.

TIRA inatoa rai kwa walioathirika ambao walikuwa na kinga ya bima inayohusiana na tukio hili kuzitaarifu mapema kampuni zao za bima na kufuata taratibu za kuwasilisha madai, ikiwemo kuwasilisha nyaraka zinazohitajika. Kampuni za bima zinazohusika zinatakiwa kuwaelekeza wakatabima kuhusu taratibu hizo, kuwajulisha hatua iliyofikiwa na kushughulikia madai yao kwa haki na kwa wakati.

Aidha, TIRA inatoa rai kwa wananchi kote nchini, wakiwemo wenye nyumba, mali nyingine na wamiliki wa biashara, kukata bima inayolingana na hatari zinazoweza kuathiri mali na shughuli zao. Wananchi wanahimizwa kupata elimu na ushauri kutoka kwa washauri wa bima na watoa huduma wengine wa bima ili waelewe aina za kinga zinazopatikana na masharti yake, na waweze kuchagua bima inayokidhi mahitaji yao.

MAKAO MAKUU
TIRA BIMA HOUSE, Njedengwa,
S. L. P. 2987, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 (026) 232 1180
Nukushi: +255 (026) 232 1180
Barua pepe: coi@tira.go.tz
Tovuti: www.tira.go.tz

OFISI NDOGO – ZANZIBAR
TIRA BIMA HOUSE, Mtaa wa Kilimani,
S. L. P. 133, Zanzibar.
Simu: +255 (024) 223 7272
Nukushi: +255 (024) 223 7272
Barua pepe: dcoi@tira.go.tz
Tovuti: www.tira.go.tz

OFISI NDOGO - DAR ES SALAAM
TIRA BIMA HOUSE, Mtaa wa Mtendeni,
S. L. P. 9892, Dar es Salaam.
Simu: +255 (022) 213 2537
Nukushi: +255 (022) 211 6120
Barua pepe: col@tira.go.tz
Tovuti: www.tira.go.tz

Huduma hizi zinapatikana katika maeneo mbalimbali nchini kupitia watoa huduma waliosajiliwa na TIRA na wenye leseni hai. Taarifa zao zinapatikana kwenye tovuti ya TIRA, www.tira.go.tz.

TIRA itaendelea kufuatilia namna madai yanayohusiana na tukio hili yanavyoshughulikiwa ili kuhakikisha haki na maslahi ya watumiaji wa huduma za bima yanalindwa. Wakatabima wanaohitaji mwongozo au wanaopata changamoto katika kushughulikiwa kwa madai yao wanaweza kuwasiliana na TIRA.

Imetolewa na



HADIJA I. MAULID,

MENEJA UHUSIANO NA MAWASILIANO KWA UMMA.

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA (TIRA)